

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Anwani ya simu: 'SIASA'  
Simu: 026 2137232  
Fax: 026 2136924  
Tovuti: www.orpp.go.tz



Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa  
Viwanja Vya Nanenane Nzuguni  
Jengo la Wizara ya Kazi,  
Mtaa wa Nzuguni A  
P.O. Box 2851  
**DODOMA**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MAOMBI YA USAJILI WA MUDA WA CHAMA CHA SIASA "UMOJA PARTY"**

Leo tarehe 19 Aprili 2022, baadhi ya vyombo vya habari vya hapa nchini vimeeleza kuwa, chama cha siasa "Umoja Party" kimepata usajili wa muda. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa tunatumia fursa hii kuwafahamisha kuwa, chama hicho cha siasa kimewasilisha maombi ya usajili wa muda na maombi hayo bado yanafanyiwa kazi, hivyo bado hakijapata usajili wa muda.

Vilevile, kuna picha katika mitandao ya kijamii za watu wanaosemekana kuwa ni wanachama wa chama hicho, wakionekana wamevaa fulana zenye bendera ya chama hicho na picha ya Kiongozi ambaye siyo mwanachama wao.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inatumia fursa hii pia, kuwakumbusha wanaotengeneza, wanaovaa fulana hizo na Watanzania wote kwa ujumla kuwa, ni kosa la kisheria kwa taasisi yoyote kufanya kazi kama chama cha siasa wakati siyo chama cha siasa kilichosajiliwa. Kwa maana hiyo, ni kosa kwa chama cha siasa kilichowasilisha maombi ya usajili wa muda, kufanya kazi kama chama cha siasa wakati hakijapewa cheti cha usajili wa muda. Kifungu husika cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 kinaeleza ifuatavyo, nanukuu:-

*"7(3) No organization shall operate or function as a political party unless it has first been registered in accordance with the provisions of this Act."*

Hivyo, mtu yeyote anayefanya siasa kwa kutumia jina "Umoja Party", bendera, nembo au alama yoyote ya chama hicho, anakiuka Sheria na anapaswa kuacha mara moja. Aidha, waanzilishi wa chama hicho wanashauriwa kuendelea kufuatilia maombi ya usajili wa muda waliyowasilisha.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Sisty L. Nyahoza'.

Sisty L. Nyahoza

Kny: **MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

19 Aprili 2022